# AFRI TWENDE

Kulitia moyo Kanisa kwa ajili ya kazi ya Umisheni wa Kiulimwengu

Juzuu ya 4 Toleo la 4



## UHAMASISHAJI

### Kutana na wanaume na wanawake ambao wanahamasisha na kuandaa kanisa la Afrika kwa ajili ya kazi ya umisheni

- Uhamasishaji kupitia safari za umisheni za muda mfupi
- Rasilimali kwa ajili ya uhamasishaji
- Uhamasishaji kupitia maombi

# YALIYOMO











## 03 MAONI YA UHARIRI

## 04 WANA NA MABINTI ZA AFRIKA: AMKENI NA KUMWOMBA BWANA WA MAVUNO

Kanisa katika Afrika linachukua nafasi yake katika kuendeleza kazi ya umisheni ulimwenguni. Lakini hatua ya kwanza na ambayo ni muhumu zaidi siyo kununua tiketi ya ndege; bali ni kumwomba Bwana wa mavuno.

## 05 UHAMASISHAJI KUPITIA SAFARI ZA UMISHENI ZA MUDA MFUPI

Wamisionari wengi wenye uzoefu wanaeleza kwamba safari za muda mfupi zilisaidia kuthibitisha kuitwa kwao. Soma habari za vijana watano wamishonari wenye hamasa kuhusu safari fupi nchini Msumbiji.

## 08 MHAMASISHAJI MZOEFU ASHIRIKISHA BUSARA ZAKE

Kaka Kehinde Ojo huendesha mafunzo sehemu nyingi duniani akiwa na timu ya wawezeshaji 15. Soma mikakati yake mitatu na rasilimali tatu kwa ajili ya uhamasishaji wenye matokeo!

**10 NENDA! Habari za Uhamasishaji wa Kanisa**

**12 Makundi 12 ya Watu: WAZIGUA**


© 2021 AFRITWENDE.
AFRITWENDE ni chapisho lenye lengo la kuinua ufahamu, hamasa, mafunzo na kuamsha makanisa na watu binafsi katika kuelekea kwenye huduma ya umisheni ulimwenguni.

**Mchoraji:** Pilgrim Communications

Maoni yaliyoelezwa hapa katika makala mbalimbali katika Jarida hili si lazima yawe ya mchapishaji.

Picha halisi hutumika mara chache. Majina ya bandia hutumika pale ambapo panahitajika kwa sababu za kiusalama.

www.afrigo.org/afri-twende

# KWA WAKATI KAMA HUU

Sote tunahusika kwa namna fulani katika 'sanaa' ya uhamasishaji, kutia moyo na kushawishi wengine katika mwelekeo fulani. Kutokana na mtazamo huu, kila mtu ni mhamasishaji, lakini ikiwa ni Agizo Kuu, basi huwa ni muhimu sana.

Hata hivyo, huduma ya uhamasishaji ina mwelekeo mwingine muhimu na tofauti; inabeba ufahamu na ubora wa wito wa mtu binafsi. Mhamasishaji ana msukumo wa kiroho wa ndani, wajibu na shauku ya kutia moyo, kutia changamoto na kuwaita watu wa Mungu wajihusishe na ajenda ya ufalme wa Mungu. Wahamasishaji ni wenye kuleta mageuzi, wakiwaonyesha watu kutoka 'hali ilivyo' hadi 'inavyopaswa kuwa' na kuwapa watu wa Mungu maono kwa ajili ya viwango vya juu na ajenda pana ya ufalme. Wanawatia watu msukumo wa ujasiri, kuwa na imani, na kuwa tayari kujitoa mhanga. Mhamasishaji hupata ufahamu wa kusudi la maisha yao pale wanapoona watu wa Mungu wakitoa maisha yao yote kwa Mungu na kwa kusudi lake la milele. Wahamasishaji husafiri katika mahusiano na huishi katika kutafuta kusudi la utukufu wa Mungu miongoni mwa mataifa.

Tunaishi katika kipindi nyeti katika historia ya kanisa ambapo ukristo unapitia ukuaji wa ajabu katika sehemu ya Kusini mwa dunia, ilhali unapungua kwa kasi katika mataifa ya magharibi. Wakati huo huo, utandawazi, uhamaji na misukosuko mingi ya dunia inatoa fursa za kipekee kwa kizazi hiki na hivyo kurahisisha mwingiliano wa tamaduni katika kufanya umisheni, ushirikiano wa kimkakati, na matazamio ya mavuno makubwa katika historia ya kanisa.

Kwa kweli, Mungu anaanzisha huduma ya umahamasishaji wakati huu, akiwaita wahamasishaji kutoka kote ulimwenguni kuungana na kanisa lake kwa ajili ya mavuno ya ulimwengu.

Kutoka upande wa kusini wa dunia hadi upande wa kaskazini, kutoka kwenye miji kwenda vijijini, vijana kwa wazee, wanaume kwa wanawake, wanatheolojia kwa walei, wahandisi kwa wajasiriamali- wahamasishaji wanapiga tarumbeta wakiita watu wote wa Mungu kujihusisha kikamilifu na Agizo Kuu. Wahamasishaji wa muda wote, wakiwa wamejitoa kwa kazi ya uhamasishaji kwa muda wao wote katika nguvu za Roho Mtakatifu, watakuwa wenye kuleta mabadilikoa kwa kazi ya umisheni duniani katika wakati wetu. Uhamasishaji wa bidii, usio na ukomo, na wa kimkakati ungeweza kuachilia nguvu kubwa ya umisheni unaohusisha jamii zote duniani kwa namna ambayo haikuwahi kuonekana. Tunaona mguso wa aina hii katika Afrika.

**Wahamasishaji wa muda wote, waliojitoa kwa kazi ya uhamasishaji ya wakati wote katika nguvu za Roho Mtakatifu, watakuwa ndiyo wenye kuleta mabadiliko ya umisheni wa dunia katika wakati wetu.**

Katika toleo hili la AfriTwende, utasoma habari za kusisimua za wanaume na wanawake wanaohamasisha makanisa kuamka kwa ajili ya kazi ya Umisheni katika mataifa. Utafurahia kusoma makala ya Kaka Kehinde Ojo ambaye, pamoja na mafanikio yote kwa viwango vya ulimwengu huu, aliamua kuitikia wito wa kazi bora zaidi kutoka juu! Tony na Julia, wanandoa vijana na wenye nguvu ambao nimewafahamu kwa miaka kumi, wanashirikisha ushuhuda wao wa kushangaza kama wahamasishaji wa muda wote, waliojitoa katika kuelimisha makanisa katika nchi ya Kenya kuhusika katika kazi ya umisheni duniani. Timu ya AfriTwende inachukua kurasa mbili kushirikisha rasilimali za uhamasishaji kama vile kutoa kozi za masomo ya Biblia kwa njia ya mtandao, na mengine mengi. Pia tunatoa taarifa juu ya vijana watano ambao walitumika katika safari fupi za umisheni na jinsi safari hizo zinavyoweza kuhamasisha watu binafsi na makanisa yanayowatuma.

Nafsi zenu na zihuishwe na kila mhamasishaji athibitike na kufarijika katika shughuli ya kupiga tarumbeta kwa ajili ya kazi ya Mungu ya umisheni katika bara lote la Afrika.

"Uhamasishaji ni mchakato wa kuwatia maono na kuwaelimisha watu wa Mungu kuhusu mipango yake kimkakati kwa ajili ya ulimwengu. Ni njia ya kuwahifadhi wale wanaohusika na wanaoendelea mbele mpaka wapate mahali na nafasi yao ya pekee katika ulimwengu wa uinjilisti." – Na Fred Markert, GlobalCAST Resources



*Sam Ngugi na mkewe Harriet ni waasisi na viongozi wa Ushiriki wa Kampeni ya Umisheni (Mission Campaign Network), ambao ni shirika la uhamasishaji likifanya kazi kuendeleza dhima na maono miongoni mwa wanafunzi wa vyuo na makanisa katika Afrika Mashariki. Pia walizindua GEN 12 – Shirika la Umisheni kwa ajili ya kutuma wamishonari wa kiafrika katika makundi ya watu ambao kwa kiasi kikubwa bado hawajafikiwa.*

# WANA NA MABINTI WA AFRIKA: INUKENI NA MUMWOMBE BWANA WA MAVUNO

*Kwa maana tokea maawio ya jua hata machweo yake jina langu ni kuu katika Mataifa; na katika kila mahali unatolewa uvumba na dhabihu safi kwa jina langu; maana jina langu ni kuu katika Mataifa.* (Mal 1:11).

Leo shamba la umisheni limekuwa ndiyo nguvu ya umisheni! Kanisa katika Afrika linachukua mahali pake katika kuendeleza dhima ya Mungu katika ulimwengu wa umisheni. Lakini kwa mujibu wa Yesu katika Luka 10, hatua ya kwanza na muhimu ni kufanya hili: Kumwomba Bwana wa mavuno! Si pesa nyingi au tiketi ya safari ya ndege! Yeye ndiye anayeita watenda kazi wapya na kuwaamuru kuungana naye kwa kuomba ili atume watenda kazi zaidi. Wengi wamekuja kutambua wito wao kwa Mungu baada ya wakristo wengine kuomba kwa ajili yao.

Kama Samweli Zwemer alivyowahi kusema, "Historia ya umisheni ni historia ya maombi yaliyojibiwa. Ni ufunguo kwa ajili ya tatizo lote la umisheni. Njia zingine zote za kibinadamu ni kitu cha pili." Zwemer alikuwa ni mmishonari wa kwanza wa muda mrefu aliyefanya kazi katika ulimwengu wa kiarabu, akitumika kutoka mwaka 1891 hadi 1929, na alipewa jina la utani kama mtume wa Uislamu. Katika hekima ya Mungu inayopita zote, alibuni shughuli ya umisheni kuwa ndiyo moja ya kitu pekee cha kumtegemea Mungu katika maombi. Mungu hukamilisha makusudi yake katika majibu kwa maombi ya watu wake.

Kanisa la Afrika linajulikana kama kanisa linaloomba. Linamiliki rasilimali hii muhimu inayohitajika kwa maendeleo ya Umisheni wa Mungu duniani. Lakini rasilimali hii inahitaji kuelekezwa zaidi kwenye maendeleo ya kazi ya Umisheni wa Mungu kupitia maombi na maombezi kwa wamishonari na kwa watu ambao bado hawajafikiwa.

Mungu anawaita wengine kwenda na wengine kukaa, lakini anatuita sisi sote kuomba. Anawategemea wale ambao wamebaki kuhubiri mahali walipo, wakiwafanya watu kuwa wanafunzi, wakiwatuma wanafunzi na kuomba. Wale waliotumwa kwenda mbali wakati wote wanahitaji kundi la watumaji waliojitoa kusimama nao katika maombi na kuwategemeza kwa msaada wa kifedha. Kupitia maombi ya kimkakati na yasiyokoma, (Luka 11:1-10), viongozi, makanisa, wana na binti wa Afrika ambao wamo ndani ya Kristo wanaweza kuinuka. Waweza kushikamana fursa hii na heshima hii ya kuungana na Mungu katika haja hii ya heshima kwa ajili ya kumfanyia ibada kwa "kusafiri kwa magoti yetu." Nchi zinaweza kubadilika kwa sababu ya maombi yetu (angalia mfano kwenye pembezoni).

**Hudson Taylor, mmishonari chipukizi nchini China, aliwahi kusema: "Kaka, kama ungeingia jimbo lile, lazima uende mbele kwa magoti yako."**

Mmishonari Luka Herrin, Mkurugenzi wa kimataifa wa Africa Inland Mission (AIM) aliwahi kushauri, "Ombeni ili Bwana atume watenda kazi zaidi, ombeni ili Bwana atume watenda kazi kutoka miongoni mwenu (kanisa lako la mahali, kikundi cha usharika ) na ombeni ili Bwana akutume wewe." Hapa chini ni baadhi ya maswali ya kutafakari:

- Unafanya nini katika muktadha wako kuomba kwa ajili ya kazi za umisheni na wamishonari?
- Kanisa lako linafanya nini katika kuomba kwa ajili ya umisheni na wamishonari?
- Ni hatua gani mahususi unaweza kuchukua kuongeza maombi na kuunga mkono kwa wakristo kutumwa kwa waliopotea?



*Dk. Jacob Igba anatumika kama mratibu wa uhamasishaji kwa eneo la Afrika Kusini kwa Africa Inland Mission (AIM). Yeye anatoka Nigeria, uzoefu wake ni pamoja na huduma kwa vyuo vikuu, upandaji makanisa miongoni mwa mataifa ya Kiislamu ya Nigeria kaskazini, na kufundisha Agano Jipya, elimu juu ya Kristo, elimu juu ya Mungu, na umisheni. Jacob na mkewe Juliet wana watoto wawili wa kiume*

## Maombi Yaliyojibiwa

"Nilitumikia miaka minne katika Afrika ya Kaskazini pamoja na familia yangu kama mmishonari... Nchi yote ilikuwa na waislamu wengi, huku kukiwa na pengo kubwa kati ya matajiri na maskini. Polisi mafisadi waliwasumbua madereva wa teksi. Hali ya usafi haikuwepo kabisa kutokana na uhaba wa maji. Jumapili ilikuwa ni siku ya kufanya kazi kitaifa. Hali hiyo ilihitaji hatua ya haraka. Kwa hiyo, viongozi wa kikristo waliandaa orodha ndefu ya maombi ikijumuisha karibu kila hitaji la kitaifa na kukusanya watu kutoka makanisa machache ya kiinjili katika mji mkuu ili kuanza siku 40 za kufunga na kuomba kwa ajili ya vita ya kiroho."

Matokeo yalikuwa ya kushangaza. Juma lile lile tulipoanza kuomba kuhusu ufisadi wa polisi, madereva wa teksi walianza mgomo. Katika uchunguzi, serikali iliagiza polisi wote waondolewe barabarani na vizuizi vyote viondolewe ili kutoa nafuu kwa kila mtu. Pia, katika hilo juma ambalo tulikuwa tunaomba kuhusu hali ya usafi katika mji, magari makubwa ya kuzoa taka kama 50 yaliyotolewa msaada na nchi ya Israeli yalianza kuzunguka na kuzoa taka. Mshangao wetu wa mwisho ulikuja pale Rais alipotangaza kubadilisha mwisho wa juma kuwa ni Jumamosi- Jumapili. Hii ilikuwa ni nguvu ya kufunga, maombi na vita ya kiroho."

– J.F.K Mensah wa Ghana.

www.afrigo.org/afri-twende

# KUPITIA

## SAFARI FUPI ZA KIMISHENI

Tafakari kundi la vijana likisafiri pamoja kwenye mwambao wa pwani ya kaskazini ya Msumbiji. Wanatoka nchi ya Lesotho, Botswana, na Kenya. Je, hawa ni watalii? Au wanafunzi wa Chuo Kikuu kwa kazi maalum? Hapana. Hawa ni vijana wamishonari wakiwa kwenye safari fupi ya majuma manne.

Watu ambao bado hawajafikiwa, jamii ya Macua Nahara, wana imani tu ya kindugu ya kiislamu na wana mashaka sana na watu kutoka nje ya maeneo yao. Kiwango cha elimu yao ni kidogo, asilimia 20 tu ya wanaume na asilimia tano ya wanawake ndiyo wanaweza kusoma na kuandika. Wanakataa kabisa Injili.

Mwezi wa Oktoba mwaka 2019, wamishonari watano ambao hawakuwa na uzoefu wa kazi za umisheni lakini wenye moyo mkuu wa kufanya kazi za kimishonari walifika katika hali hii. Baadhi yao walikuwa na ndoto ya kuwa wamishonari kwa miaka mingi. Wengine, kama Rosy kutoka Lesotho alisikia juu ya safari akiwa kanisani: “Nilihamasika kutokana na habari nilizozisikia na kwamba nilitaka kutoka nje na kuona jinsi ambavyo nami ningeweza kutumika.” Kiongozi wa safari August Basson ni mishonari mwenye uzoefu na ambaye ndoto yake imekuwa ni kuwaandaa wamishonari wa kiafrika. Mwaka jana, aliongoza timu ya vijana wa kiume kwenda kusini mwa Tanzania, na matokeo yake – timu ya huduma ya mavuno ilizaliwa.



Wana-timu ni pamoja na August Basson wa Afrika ya Kusini, Maureen Nyambura wa Kenya, Leratho Lesoetsa wa Lesotho, Thato Mokgethi wa Botswana, Neo Moeti na RosyLangane wa Lesotho.

Kikundi kilisafiri kwenda kwenye kijiji kilichoko Pwani, kikatengeneza nyumba ya matope na kukaa huko kwa muda wa juma moja. Walijifunza baadhi ya lugha za kienyeji, walifanya shughuli za vijana, waliongoza michezo, na walijifunza na kufundisha nyimbo. Walisaidia kukaa na watoto ili mmishonari mwenye uzoefu aweze kufundisha neno la Mungu na hata kutumia mashine za kufundishia sauti za lugha ili kusaidia kufundisha watu kusoma na kuandika.

Mmishonari Grant Franke kutoka Afrika ya Kusini na familia yake wameishi na kufanya kazi katika jamii ya Macua Nahara kwa miaka minane. Alifundisha timu yake baadhi ya semi za lugha ya Macua Nahara kila siku na walizunguka katika kijiji wakifanyia mazoezi kile walichofundishwa, wakiwaalika watu kuja kwenye mafundisho ya Biblia na pia kupata masomo ya kilimo na kujifunza kusoma. Grant alisema mahudhurio yalipanda mpaka kufikia asilimia 1000 na hata wanawake ambao ni nadra kujitokeza katika jamii hiyo nao walikuja.

Vijana wadogo wa kike katika kijiji walifanya kazi zaidi na timu ya mavuno ya wanawake. Wasichana hawa wanaishi katika mazingira ambayo ni hatari sana, na kwa hiyo walijisikia salama kuwa na timu yetu. Walipowaaga, wengi wa wasichana hao walisononeka.

Grant alisema: “Ni jambo lenye matokeo mazuri sana pale Waafrika wanapokuwa wamishonari kwa Afrika. Wameweza kuaminiwa zaidi ndani ya juma moja kuliko miaka minne niliyotumia mimi”. Anasema mara kwa mara amekuwa akiulizwa kuwa lini tena timu itarudi kuwatembelea.

Kwa huzuni, kwa kawaida huwa kuna matokeo kidogo ya muda mrefu katika jamii zilizotembelewa na timu za kimisheni za muda mfupi. Wanajenga kuaminiana au kutatua matatizo ya kijamii, lakini matokeo ya muda mrefu huja katika maisha ya timu na Makanisa yao. Mwana-timu ya mavuno, Lerato alisema: “Nimekuwa nikitafakari kufanya kazi ya umishonari- sasa nina uhakika nataka kuwa mishonari wakati wote”.

Wamishionari wengi wenye uzoefu wanasema safari fupi zilisaidia kuthibitisha kuitwa kwao. Wale ambao hawawezi kwenda hugeuka kuwa watu wanaosaidia na kuwaombea wamishonari walioko kazini –kwenye shamba la mavuno. Safari fupi za kimisheni huhamasisha kanisa kuwategemeza kwa maombi na msaada wa pesa walio watuma. Safari fupi ni zana yenye matokeo mazuri kwa kuwaandaa watu kwenda, kutoa na kuomba kwa ajili ya makundi ya wamishonari duniani kote.

Je, ungetamani kuwa mmoja wa wana-timu wa umisheni wa muda mfupi? Wasiliana na August Basson kwa: august.basson@aimint.org Kujua zaidi kuhusu [Harvest Team].

Kuwaombea Macua Nahara, tembelea www.nahara.info


Mtaalam wa masuala ya vyombo vya Habari Halley McNeill akifuatana na Timu ya Mavuno. Angalia safari yao ya kusisimua kwenye Facebook: https://www.facebook.com/AIMtheharvestafrica. Itakusisimua!

# UNGEPENDA KUJIUNGA NA UMISHENI – LAKINI NINI KINAFUATA?

Timu ya AfriTwende imeweka pamoja orodha ya rasilimali ambazo zitasaidia kufahamu nini maana ya umisheni, jinsi ya kujihusisha, na namna ya kuleta watu pamoja nawe katika mpango mkuu wa Mungu wa baraka kwa ulimwengu! Kila kozi inafundisha mpango wa Mungu wa kuleta watu kwake. Kila mmoja unakuonyesha ni kwa namna gani, kupitia maandiko, Mungu ameweka kusudi kwenye taifa la Israeli na kanisa kumjua yeye, pendo lake na kushirikisha wengine neema ya wokovu wake. Lakini ipi ni sahihi kwako? Inategemea na hali yako na kule unakoelekea.


## KOZI ZILIZOFUNDISHWA NA MWEZESHAJI ALIYEPATA MAFUNZO

Kozi zifuatazo zinakamata falsafa ya **Perspectives** na zinapatikana kupitia uhamasishaji rahisi kabisa www.simplymobilizing.com . Baada ya kuhudhuria ndipo unaweza kufunzwa kuwa mwezeshaji.




Kwanza, hebu tukutane na babu wa mafunzo ya Umisheni – **Perspectives**. Hii ni kozi ya majuma 15 ambayo inahitaji mwezeshaji aliyepata mafunzo pamoja na masaa zaidi ya 50 ya darasani na kazi za kufanya nyumbani. Mafunzo haya yamehakikishwa kuwa yataleta kiwango kipya cha ufahamu wa mamlaka ya kibiblia katika kupeleka ujumbe wa Mungu kwa mataifa. Imebuniwa kwa mitazamo minne: Kibiblia, kihistoria, kiutamaduni na kimkakati. **www.perspectives.org**

**KAIROS**





Kila mkristo anapaswa kuchukua kozi ya KAIROS, hata kama tayari wana maono kwa ajili ya kuufikia ulimwengu. Kama ilivyowasilishwa na viongozi waliopata mafunzo, vipindi tisa vya kairos vinavyosisimua ni pamoja na video, makundi madogo ya majadiliano na kazi za nyumbani.

*"**Kairos** imefungua macho yangu. Moja ya vipindi kilikuwa kinahusu wakristo wa majina tu, na wale waliojitolea. Kupitia kairos, nimejifunza kwamba umisheni ni kiini cha Ukristo. Moyo wangu uwe kwa ajili ya umisheni kama moyo wa Kristo ulivyo kuwa kwa ajili ya umisheni. Labda sijajitoa kama ambavyo nilifikiri kama sijajitoa kwa moyo wa ukristo, ambao ni umisheni. Hii imenipa changamoto ya kuomba, siyo kwa ajili yangu na wale wanaonizunguka, bali pia kwa ajili ya mataifa," anasema Sarah.*


*(Sarah ni mwanafunzi wa mwaka wa tatu katika fani ya udaktari wa familia.)*




**Youth KAIROS**
[Vijana wa KAIROS]
Hii ni kwa ajili ya vijana wenye umri kati ya miaka 16 na 20. Kozi hii huwasilishwa na mwezeshaji kwa siku tatu na nusu. Inahifadhi maono na uvuvio wa kozi ya KAIROS.
www.facebook.com/youthkairos




**The Unfinished Story**
[Hadithi isiyokamilifu]
Kama Kairos, TUS inafuatilia mapana ya kazi ya umisheni wa Mungu kutoka kitabu cha Mwanzo hadi vitabu vya Injili, na kwa muda wa miaka 2000 ya vuguvugu la kikristo ulimwenguni. Makanisa ya mahali yanaweza kuitumia kama vile shule ya Jumapili au darasa la kujifunza Biblia. Kuwa kiongozi wa TUS unahitaji kuhudhuria darasani na kuwa na saa chache za mafunzo. TUS inaunda mtazamo wetu wa ulimwengu wa kibiblia ili tuone ushiriki wetu pamoja na Mungu katika huduma kama hali ya kusisimua na ya maana katika kumfuata Yesu!




**Empowered to Influence**
[Kuwezeshwa Kushawishi]
Kozi hii ya vipindi vinne imewezeshwa kwa kutumia video ya mfanyabiashara wa Singapore anayeitwa Ken Chua. Mafundisho yake yamejikita kwenye njia mpya saba za kufikiri zinazohitajika ili waumini kuwa washawishi kwa ajili ya Mungu katika maeneo yao ya kazi, kanisani na nyumbani. Ingawa inafaa zaidi kwa wafanyabiashara, lakini itamwezesha kila mwamini kuzitumia.


**Interface** [Mwingiliano]
Kozi ya "Interface" kinajibu swali hili: "je, kanisa lililojiunga na umisheni pamoja na Mungu linaonekanaje?" Utangulizi wa uwasilishi unafuatwa na semina ya siku moja au warsha ndefu. Inavumbua muundo wa kanisa ambao utalea, utaandaa na kuruhusu watu wa Mungu katika huduma inayoleta mazao.

Kwa taarifa zaidi kuhusu lini na wapi unaweza kupata kozi hizi, wasiliana na:
**Afrika Mashariki:** samuangugi@gmail.com

## MASOMO YA BURE AMBAYO YANAPATIKANA KUTOKA KWENYE MTANDAO NA UNAWEZA KUJIFUNZIA NYUMBANI


**XPLORE**
Masomo haya saba ya kundi dogo la kujifunza yanawakilisha taarifa ya sasa juu ya hali ya Ukristo ulimwenguni, sambamba na makundi ya watu ambayo bado hayajafikiwa na Injili ya Kristo pamoja na dini nyingine kubwa. Kinafundisha tabia tano ambazo waumini wote wanaweza kuziweka katika matendo na kubadilika kuwa wakristo wa ulimwengu.
www.mobilization.org/resources/live-missionally/xplore/




**Go Mobilize**
[Nenda Uhamasishe]
Hatua hii nyingine inafundisha kile kinachotakiwa kwa mtu ambaye ni mhamasishaji na jinsi ya kuanza vuguvugu la umisheni miongoni mwa rafiki zake na mawasiliano yake. Masomo haya ni pamoja na namna ya kutumia maandiko kuwaonyesha wengine shauku ya Mungu kwa kila taifa, na jinsi ya kuwaelekeza wengine mahali ambapo bado hakuna injili au uwezekano wa kuingia ni mdogo.
www.mobilization.org/resources/mobilize-others/go-mobilize/

**Your Church Can Change the World**
[Kanisa lako laweza kubadilisha dunia]
Kitabu hiki cha mafunzo ambacho hutolewa bure kinaweza kuboreshwa kulingana na muktadha wako. Kimeandikwa nchini Mexico na kimekusudiwa kwa ajili ya wakristo waliokomaa kiimani, na baadhi ya sehemu za kitabu hicho zinaeleza "Kwa nini Kanisa Linapaswa kujihusisha na umisheni, kuomba kwa ajili ya ulimwengu, mahitaji ya fedha kwa ajili ya kazi za umisheni na kamati za umisheni katika Kanisa la Mahali.
www.yourchurchcanchangetheworld.org/




Kama una shauku kuhusu umisheni na unataka kuona wengine wakitambua uwezo wao wa kwenda, kuomba au kutegemeza kifedha, basi unaweza kuwa mhamasishaji. Shirikiana na mashirika yaliyoko katika eneo lako au uwasiliane na simplymobilizing:
simplymobilizing.com/mobilizers/mobilizer-pathways/

## NYENZO/VIFAA VYA MAFUNZO

*Sehemu ya kuhamasisha ni mafunzo kwenda nje au kutumika pale ulipo. Vifaa vingi vinapatikana, ingawa wengi wanahitaji kujisajili kwenye program. Hapa kuna rasilimali chache za bure ambazo unaweza kutumia katika muktadha wako.*

**Go-er Groups**
[Makundi ya Wanaotaka Kwenda]
Somo hili hutolewa bure kwa mfululizo wa vipindi saba kwa njia ya video kwa wanafunzi walioko kwenye maeneo ya mijini. Somo hili linaibua maswali makuu na vikwazo ambavyo wakristo wanakumbana navyo wanapokuwa wanafanya huduma katika tamaduni tofauti tofauti. Video hizi zenye mtiririko wa masomo zina ushauri mzuri kutoka kwa watu wenye uzoefu. Zitumie kufanyia kazi masuala ya msingi wakati ukifikiria kuwa mmishonari.
www.mobilization.org/resources/prepare-for-ministry/








**Crossing Cultures**
[Kuvuka Mipaka ya Utamaduni]
Waamimi wengi hutamani kuwafikia watu katika jamii zao ambazo zina tamaduni au dini tofauti lakini wanakuwa waoga kutokana na kukosa uzoefu, maarifa au stadi. Warsha hii ina shughuli za kufurahisha na za kuwaandaa watu ili waweze kuwasiliana na watu katika tamaduni zingine – stadi inafaa nyumbani na mahali pote duniani. Mshirika wa kanisa anaweza kuongoza kazi hii baada ya muda mfupi tu wa mafunzo.
www.simplymobilizing.com/courses/crossing-cultures/

**Encountering the World of Islam**
[Kukabiliana na Ulimwengu wa Uislamu]
Watu wengi ambao bado hawajafikiwa na Injili ya Yesu Kristo ni Waislamu, na bado Wakristo wengi wanafahamu kidogo sana kuhusu historia au imani za dini ya kiislamu. EWI ni kozi iliyowezeshwa ambayo inaweza kukupa mwanga na maarifa katika ulimwengu wenye migongano, na kujua habari za zamani zinazohusu miungu ya Kiislamu. Utajifunza namna ya kuwaombea, kuanzisha mahusiano nao, na namna ya kuwafikia Waislamu walio karibu nawe. Madarasa yapo nchini Ethiopia, Kenya, Nigeria, Afrika Kusini na Rwanda.
info@ewi.org
www.encounteringislam.org

**Let's Go!** [Twendeni]
Kitabu cha shirika la SIM kisemacho "Na Twende!" ni kitabu kinachosadia kufahamu namna ya kuanza mahusiano na mtu, ingawa hakichukui nafasi ya mafunzo rasmi, lakini ni kitabu kinachotoa mafunzo kwa vitendo, kufanya mafunzo yawe na maana zaidi kwa mtumiaji. Kuna simulizi na shuhuda, vipeperushi, makala, Biblia za kujifunzia, na video fupi za kihabari zimetengenezwa ili ziweze kusomwa pamoja na mshauri/mwelekezi kwa muda wa miezi sita mpaka 12.




Zinaweza kupatikana kwenye mtandao:
- bit.ly/LetsGOpdf – PDF version
- bit.ly/LetsGOsupplemental – supplemental material
- bit.ly/LetsGoVideos – videos for the chapter.

www.afrigo.org/afri-twende

# MHAMASISHAJI MZOEFU ASHIRIKISHA UFAHAMU WAKE

NA MERCY KAMBURA



Kehinde Ojo alikuwa miongoni mwa wanafunzi bora wa chuo kikuu alichosoma, akisomea uhandisi wa umeme na elekroniki. Pia alichaguliwa kuwa sehemu ya menejimenti, akijifunza kazi za uongozi katika moja ya makampuni makubwa ya mafuta yaliyokuwa yanalipa vizuri sana nchini Nigeria.

Akiwa mtu anayejifunza kazi za kiwandani, aliahidiwa kazi katika kampuni hiyo, kazi ilioangazwa taaluma yake ya maisha bora ya uhakika. Lakini baada ya kumaliza mafunzo, Ojo hakurudi. Miaka miwili baadaye aliwatembelea marafiki zake waliokuwa wamepata kazi. Walishangaa sana! Ni nani mwenye akili timamu angeweza kuachia fursa kama hiyo ipotee? Ojo aliwatangazia wale wenzake kwa kusema: "Nimepata kazi bora zaidi."

Kehinde alikubali wito wa kumtumikia Mungu katika Ushirika wa Kimataifa wa Wanafunzi wa Makanisa ya Kiinjili (International Fellowship of Evangelical Students-IFES). Nafasi yake ilikuwa kuwafanya wanachuo kujua masuala ya Uanafunzi, na uhamasishaji kuhusu umisheni miongoni mwa wanafunzi waliokuwa wanaishi vyuoni.

Leo Kehinde ni mkufunzi, mtaalamu, na mshauri. Baada ya miaka 20 akiwa na IFES Nigeria, Kehinde alialikwa na IFES kuanzisha mpango mpya wa kiulimwengu kusaidia vuguvugu za kitaifa ndani ya IFES ili iweze kujitegemea kupitia harambee za kuchangisha fedha na kuifanya iweze kuwa na matokeo mazuri. Katika kuandaa mpango wa kazi, Kehinde alitengeneza timu ya kimataifa kufanya kazi naye. Anafundisha na kuandaa viongozi Afrika, Ulaya-Asia, Caribbean, Marekani ya Kusini, Asia ya Mashariki na kanda za kusini mwa Asia. IFES imetoa msaada kwa mashirika mengine katika sehemu mbalimbali za ulimwengu katika jitihada zao za kutaka kujitegemea.

Akiwa na timu ya wakufunzi 15 kutoka sehemu mbalimbali duniani, Kehinde huendesha mafunzo katika nchi kadhaa kila mwaka. Hakuna kona ya ulimwengu ambayo haijulikani kwake, baadhi ya sehemu hizo ni kama Fiji, Vanuatu, Guyana, Jamaica, Nepal, na Gambia.

## Mikakati Mitatu

Ili kuwa na uhamasishaji wenye matokeo mazuri, Kehinde anashauri mikakati mitatu mikuu kwa mhamasishaji:

**1. Uthibitisho/Uhalisi furaha**

"Mkakati wenye matokeo kwa mhamasishaji yeyote unapaswa kuwa na uthibitisho wa ukweli," anasema, Kehinde. Hili ni jambo moja ambalo linaleta mafanikio kila wakati. Kama mhamasishaji, watu wanataka uwe mkweli. Kizazi cha vijana kinataka kukuona wewe unaishi maisha halisi na unatumia kanuni zile ambazo unawasihi wao wazifuate."



**2. Uthabiti/ Kutobadilika**

"Ishi kwa kufuata kanuni unazofundisha na shikilia maono uliyonayo. Maandiko hayapitwi na wakati. Uendelee na kweli zako za kibiblia na kuwaonyesha watu wito usiobadilika katika umisheni."

**3. Usiagize matendo, uliza maswali**

"Njia inayooonekana kana kwamba ni bora ya kuwajulisha watu maono yako ni kwa kusimulia maisha yako. Hata hivyo, huenda watu wasitambue uzoefu wako na wanaweza kukosa

www.afrigo.org/afri-twende

kuona jinsi wanavyoweza kuchangia katika maono yako. Badala yake, waache watu wajihusishe kutokana na hali halisi waliyonayo- kwa namna inavyoweza kufaa kwao. Hili likiwa katika akili zao, wanaweza kutoa jibu."

## Nje ya Chuo Kikuu

Kehinde alikulia kusini magharibi mwa Nigeria. Licha ya kuzaliwa katika familia ya kikristo na kubatizwa siku ya nane tu baada ya kuzaliwa, aliyatoa maisha yake kwa Krsito alipokuwa Chuo Kikuu. Haikuwa ni wokovu tu alioupata katika miaka hii akiwa mwanafunzi wa Chuo Kikuu, bali pia alipata wito wa maisha yake. Hii ilitokea juma moja tu kabla ya kufanya mtihani wake wa mwisho.

"Sikuwa na raha Jumapili hiyo, niliacha hata ibada nikaenda kuomba peke yangu kwenye bustani." Alihisi kwamba mwelekeo wa maisha yake ulikuwa kwenye ukingo wa kubadilika, lakini hakuweza hata kuelewa. Wakati wa ibada, Mungu alizungumza kupitia mhubiri kwamba miongoni mwa wahitimu wa Chuo Kikuu, Mungu alikuwa anamwita mmoja wao kumtumikia.

"Ni mimi tu nilitokea mbele siku hiyo; hapakuwa na kuchanganyikiwa hata kidogo," anaongeza. Miaka 31 baadaye, chaguzi za maisha yake yote zimechongwa na uamuzi huo mmoja.

## Rasilimali Tatu

Kwa muda wa miaka tisa iliyopita, jukumu la Kehinde limekuwa ni kuhamasisha na kuandaa harakati ya kitaifa ya IFES kukubali manufaa ya kujitegemea kwa kutumia rasilimali ziliziko katika mazingira yao. Hii hufanyika kupitia tafiti, mafunzo, ushauri/ufundishaji, na kupanga ruzuku zinazoendana. Kama mhamasishaji, Kehinde husisitiza rasilimali tatu ambazo wakristo wanaweza kuzitumia kupeleka injili mbele.

**1. Muda**

Kitu kinachomsawazisha kila mtu ni muda! Sote tuna muda ulio sawa. Ni kwa jinsi gani washirika ambao hawana fedha au stadi wanaweza kutumia muda wao kutumikia huduma?



Kimsingi wanaweza kutumia sehemu ya muda wao kuomba kwa ajili ya umisheni na kutembelea washirika katika umisheni.

**2. Talanta**

Wengine wana stadi na wana uwezo mkubwa katika taaluma zao. Watu hawa wanaweza kujitolea kufanya kazi kwenye huduma na kutoa huduma ambayo isingepatikana bila kulipiwa.

**3. Hazina**

Aina ya hazina inaweza isiwe na muda au kipawa kuwepo, lakini wanaweza kutoa rasilimali kama pesa au vitu ambavyo vinaweza kusaidia mahitaji ya shirika. "Rasilimali za muda, talanta, na hazina ziko kila mahali! Kwa miaka mingi, viongozi wengi wa huduma wamejielekeza kwenye uhamasishaji wa pesa, huku wakiacha rasilimali zingine. Viongozi wanahitaji kufungua rasilimali hizi zingine ambazo zinapatikana katika mazingira yao na kuziachilia kwa ajili ya maendeleo ya huduma," anasema Kehinde.

Je, kwa miaka 29 baadaye, Kehinde amejuta uamuzi wa kujiunga na uanafunzi na uhamasishaji wa shughuli hii? La, hasha!

"Sijawahi kuacha kutumia maarifa yangu ya uhandisi na stadi hata katika kazi yangu ya sasa; bado natumia kanuni za uhandisi kufanya maamuzi". Maneno katika 1 Nyakati 29: 1 yameendelea kuwa faraja kwangu. Mfalme Daudi aliuambia mkutano: "Mwanangu Sulemani, ambaye Mungu pekee aliyemchagua, ni kijana mdogo na asiye na uzoefu; na kazi ni kubwa."

www.ifesworld.org




# NENDA! HABARI ZA KUHAMASIKA KWA KANISA LA AFRIKA

## A Retrospect: The Story Behind My Zeal for Missions

Imeandikwa na J. Hudson Taylor

[Kuangalia nyuma: Hadithi kuhusu ari yangu ya Umisheni]
Hudson Taylor anatambulika kimataifa kama baba wa imani katika vuguvugu la umisheni. Kitabu hiki kidogo, kinachopatikana bure, kinasimulia hadithi kwa maneno yake mwenyewe jinsi alivyosikia wito na kuondoka nyumbani kwake huko




Uingereza na kwenda China. Anasimulia hatua alizochukua kujifunza kumtumaini Mungu pekee kwa ajili ya mahitaji yake katika nchi ya kigeni. Mfano na ushuhuda wake utakutia moyo wewe msomaji kuanza kukimbia mbio zako kwa subira pia kama Hudson alivyofanya. Mara kwa mara, Mungu alilinda maisha yake na alifungua milango kwa ajili yake. Kitabu hiki kinapendekezwa kusomwa na kila mtu anayetaka kuvuviwa na kutiwa moyo katika safari yake ya imani!
Kinapatikana kwenye maduka ya Amazon hapa:
https://amzn.to/2OmK4rZ

## Global Prayer Digest




[Muhtasari wa Maombi kwa Ulimwengu]
Je, unataka kuomba kwa ajili ya watu ambao bado hawajafikiwa na Injili lakini huna uhakika ni wapi utakapopata taarifa hizo? Njia rahisi ya kugusa umilele kupitia maombi ni kutembelea tovuti ya Muhtasari wa Maombi kwa Ulimwengu. Kila siku, taarifa na mwongozo wa maombi kwa ajili ya Makundi ya Watu ambao bado Hawajafikiwa unawekwa kwenye tovuti. Kila mwezi, mada tofauti inayohusiana na dini mbalimbali za watu ambao bado hawajafikiwa huchambuliwa katika makala.
www.globalprayerdigest.org/. Kujiunga, tazama chapisho na jiunge katika maombi haya pamoja na wengine.

## Chama cha kwanza cha Kikristo cha waandishi wa Habari kwa nchi za Afrika zinazozungumza Kifaransa



Tukio la kihistoria lilishuhudiwa mwezi Septemba 2019 ambapo chama cha Kikristo cha waandishi wa Habari wanaotumia lugha ya Kifaransa kiliundwa. Hii ilitokea wakati wa utambulisho wa jarida kwenye kongamano la mafunzo lililofanyika katika Jiji la Abdjan nchini Ivory Coast. Chama hiki kipya kitakuwa faraja kwa majarida na magazeti ya kikristo kama sauti katika jamii zao.

Maono ya kuanzishwa kwa chama hiki yaliwasilishwa na Dk. Jules Ouoba, Mkurugenzi wa kituo cha Machapisho cha Kiinjili huko Abidjan, ambacho kimeshirikiana na shirika la kimataifa la mafunzo ya Majarida kufanya hili kongamano. Kusanyiko la watu wapatao 100 walipiga kura na kumchagua Guy Irie (kulia) kuwa Rais; Tshanyi Mutshuka Israel (kushoto) kuwa Katibu Mkuu; na Hillary Honore (katikati) kuwa Mtunza Hazina.



## Baba wa Umisheni Nigeria Afrika

Mchungaji Panya Baba amefariki na kwenda zake mbele ya Muumba siku ya Jumamosi, 19 Oktoba 2019. Mchungaji Baba alianza kazi yake ya umishonari akiwa na umri wa miaka 17. Alikuwa Mwasisi wa Vuguvugu la Kimisheni la Kiinjili la Nigeria (Nigeria Evangelical Missions Association (NEMA), Mkurugenzi wa chama cha kimisheni cha Kiinjili cha kanisa la ECWA, na Rais wa madhehebu ya ECWA nchini Nigeria. Miaka sabini baada ya kazi yake alikuwa ameshabadilisha sura ya umisheni ndani ya Afrika ya Maghribi. AfriTwende Toleo 4, Na 2, lina makala kuhusu kazi yake na maisha yake.
www.bit.ly/37RL8fc



# WAMEITWA:
## TONY NA JULIA MBURU

Mungu anapokuonyesha anachofanya, ni mwaliko wa moja kwa moja kwamba anataka uungane naye. Maneno haya kutoka kwenye darasa la kujifunza Biblia yalikuwa ni ufunuo mkuu kwangu. Hata hivyo uamuzi wangu kufanya kazi kama mhamasishaji na mmishonari ulikuwa ni mchakato, si kama vile aya moja inavyotoka kwenye ukurasa wa Biblia. Nilijua kuwa nilitamani kumtumikia Mungu; lakini sikujua ni kwa vipi.

Tulipoanza kusikia wito wa Kimakedonia, tulikuwa bado hatujaoana na ulikuwa ni uamuzi mgumu. Nilikuwa tu nimemaliza masomo yangu ya uhandisi wa umeme na elekronikisi kutoka Chuo Kikuu cha Kilimo na Teknolojia cha Jomo Kenyatta, (Jomo Kenyatta University of Agriculture and Technology) wakati Julia alikuwa mwaka wake wa mwisho wa kusomea Teknolojia ya Habari. Tuliweka mipango kwa yale tuliyotaka kufanya. Hatukutaka kujihusisha na kazi ya Uhamasishaji kwa muda wote.

> Kama wahamasishaji, sisi pia, tunapuliza tarumbeta la wazi kabisa kwa kanisa na kutangaza kuwa ni wakati kwa Afrika kuinuka na kupeleka Injili kwa ulimwengu.

Tulifanya kozi ya KAIROS pamoja mwaka 2010, ilikuwa dhahiri nini nilitaka kufanya- kuhamasisha umisheni! Kupitia kozi hiyo, Mungu alitusaidia kushinda hali ya kuwa na hofu ya maisha. Tuliingia kwenye huduma ya muda wote pamoja na Mtandao wa Kampeni ya Umisheni [Mission Campaign Network (MCN)].

Kuhamasisha watu kwa umisheni ni sawa na kutabiri. Manabii waliita watu kurudi kwenye kusudi la Mungu. Kimsingi tunarudi kwenye kusudi halisi la kuishi kwetu-kueneza Injili hadi kwenye miisho ya dunia, kuwa kama Kristo, na kuunda Amani (shalom) katika nchi, miji na vijiji. Kuhamasisha siyo tu kwa ajili ya makundi ambayo hayajafikiwa, ingawa ndiyo hasa yanayopewa kipaumbele. Ni kuhusu kuona utukufu wa Mungu katika kila eneo la jamii.

Katika Agano la Kale, manabii wangeweza kupiga tarumbeta kuonya au kutoa ujumbe muhimu. Kama wahamasishaji, tunapiga tarumbeta kwa uwazi kwa kanisa na kutangaza kwamba ni wakati kwa Afrika kuinuka na kupeleka injili kwa ulimwengu. Katika MCN, tunahamasisha kanisa kuchangamka katika kufanya umisheni.

Kila mwamini anatiwa moyo kuhamasisha, kwenda kama mmishonari au kuwezesha watu walio tayari kwenda, wawe wanasaidiwa kama kusaidia kulea wamishonari au kama wanataaluma na watengeneza mahema. Pia tunasisitiza jukumu muhimu la maombi kwa ajili ya umisheni.

Mafunzo ya MCN huanza na semina fupi ya masaa mawili-matatu kuwaonyesha watu kwamba umisheni ni msingi wa Biblia. Tunasisitiza kile kilichokwishafanyika sasa na kile ambacho bado hakijafanyika. Tunashirikiana na kila sehemu ya mwili wa Kristo iliyo tayari na mashirika mengine ambayo yanayo shughuli kama za kwetu ndani na nje ya Afrika. Kozi zetu hazijatengenezwa na MCN bali na washirika wetu kama vile Simply Mobilizing International, the Center for Mission Mobilization, na Perspectives. Pia tunafundisha namna ya kukabiliana na ulimwengu wa Kiislamu.

Kutoka mwaka 2011 hadi 2018, tulifanya kazi Nairobi, Kenya tukiendesha kozi za KAIROS kwa wanafunzi wa vyuo vikuu zaidi ya 1000 na Makanisa.

MCN imekuwa siku zote ikitamani uhamasishaji kutokea huko Mombasa, mji ulioko pwani ya Kenya ambao wakazi wake ni nusu kwa nusu kati ya Wakristo kwa Waislamu. Wengi wao ni Waswahili na Waarabu. Wakristo wengi hawajui namna ya kuwafikia waislamu – hata hawajui kama wanapaswa kuwafikia. Tulialikwa kuanzisha uhamasishaji na tulikubali, tukaingia huko mwaka 2018.




Kwa kazi ya umisheni, na hasa kazi iliyobakia ya kuuhubiria ulimwengu, uhamasishaji ni kitu cha kimkakati kilichobakia kwa ajili ya uinjilisti kwa ulimwengu. Kanisa linahitaji kukamilisha kusudi la kuwepo kwake. Swali ambalo tungependa kila mtu kujiuliza ni hili, "Ni nini sehemu yangu katika umisheni?"

www.missioncampaignnetwork.org

www.afrigo.org/afri-twende




# MAKUNDI YA WATU: WAZIGUA

Wazigua ni jamii ya watu wenye asili ya kibantu wanaoishi katika ukanda wa pwani ya kaskazini-masharikki mwa Tanzania. Lugha yao ni Kizigua, na pia wengi wao wanazungumza Kiswahili viziuri.

Baada ya kukimbia biashara ya utumwa huko mashariki, Wazigua waliweka makazi yao karibu na Dar es Salaam. Historia ya Wazigua ni ya zamani. Leo hii idadi yao ni kama 631,000 hivi. Nchini Tanzania Wazigua bado wanahesabika kama ni miongoni mwa makundi ya pembezoni, wakiwa bado ni jamii ya watu wenye kiwango kidogo cha elimu.

Dini yao kuu ni Uislamu ukiwa umechanganyika na mapokeo ya tamaduni za kuabudu mizimu au roho za mababu zao. Mara nyingi watoto wao hupelekwa kusoma elimu ya Kiislamu yaani madrasa. Idadi ya wakristo miongoni mwa Wazigua ni ndogo sana isiyozidi asilimia tisa.

Wazigua ni jamii yenye undugu wa karibu. Wanaishi pamoja katika vibanda vilivyokandikwa kwa matope na kuezekwa kwa nyasi na vilivyo kwenye kundi moja la pamoja. Maisha yao yanategemea ukulima mdogo na uvuvi. Kama ilivyo kwa miji mingi ya pwani ya Tanzania, zao lao kubwa la biashara ni mkonge na mazao makuu ya chakula ni mahindi na ufuta.

Wamisionari wamekuwa wakiwafikia Wazigua kwa miaka mingi. Katika mwaka 2017, Africa Inland Mission (AIM) ilianza kazi katika eneo jipya kwa mtazamo wa kuwahubiria Injili Wazigua na kuboresha maisha yao. Kazi ya kufasiri, kwa maana ya Agano Jipya na Filamu ya Yesu sasa zinapatikana katika lugha ya kizigua. Unaweza kujifunza zaidi: https://prayafrica.org/project/zigua-of-tanzania/

## Mtazamo wa Haraka- Muhtasari

- Wazigua walikimbia utumwa na kisha kuweka makazi yao katika pwani ya Tanzania. Idadi yao ni kama 631,000 hivi.
- Dini yao kuu ni Uislamu, ukiwa umefungamanishwa na mila za asili na ibada za mababu zao. Wakristo ni kama asilimia tisa tu.
- Ni moja ya makundi ya pembezoni wakiwa na kiwango cha juu cha kutojua kusoma na kuandika na ukosefu wa ajira.
- Kazi ya kutafsiri mpaka sasa imetoa Agano Jipya na Filamu ya Yesu.

## Omba

- Kwamba kazi ya Injili inayoendelea izae matunda.
- Wazigua wapate uhuru wa kweli katika Kristo kutoka kwenye dini za asili na ibada za mababu zao.
- Kwamba watenda kazi waende maeneo ya Uzigua na kuishi huko, ili kuwahubiria injili kwa moyo, kwa maneno na kwa matendo.
- Waamini wapya waweze kudumu katika imani na kuanza kuzifikia familia na jamii kubwa ya wazigua.

SIM By Prayer | AFRICA INLAND MISSION

**AFRITWENDE**: afrikatwende@afrigo.org **AFRIGO**: afrigo_english@sim.org **ALLONS-Y !** : info@afrigo.org

| SIM East Africa | SIM West Africa | SIM Southern Africa | AIM International |
|---|---|---|---|
| Tel: +251 911 206 530 | Tel: +233 30 222 5225 | Tel: +27 21 7153200 | amc.io@aimint.org |
| east-africa.office@sim.org | wamo.personnel@sim.org | za.enquiries@sim.org | aimint.org/africanmobilization/ |